



Australian Government

## COVID-19 VACCINATION

# Baada ya chanjo yako

### Madhara ni nini?



Baada ya kuwa umepata chanjo yako, unaweza kujisikia **madhara** mengine.

Madhara ni kitu kinachoweza kutokea wakati mwingine kwa watu baada ya kutumia dawa.

Madhara hayatokei kwa kila mtu.



Madhara mengi hayatakufanya uwe mgonjwa sana. Tunayaita **madhara ya kawaida**.

Lakini madhara mengine yanaweza kuwa makubwa.

Madhara hayo ni **adimu sana**.

## Madhara



Madhara mengi:

- sio ya hatari
- yanakwisha yenyewe katika siku 1 hadi 2.

Madhara mengine ya **kawaida** ni pamoja na:



- maumivu au kuvimba kwenye mkono wako mahali ambapo sindano iliingia
- homa
- maumivu kwenye misuli au maungio
- uchovu
- maumivu ya kichwa
- homa ya baridi.



Madhara **adimu** yanajumuisha:

- uwekundu au muwasho kwenye mkono wako mahali ambapo sindano iliingia
- kuhisi kama unaweza kutapika
- kujisikia vibaya tumboni



- mabonge kwa shingo yako
- maumivu katika mguu wako
- kutolala vizuri.

## Athari za kuzia



Watu wengine wanaweza kupata **athari ya kuzia (allergic reaction)** kutokana na chanjo.

Athari ya kuzia ni wakati mwili wako unaathirika kutokana na kitu, kama chakula au dawa. Kwa mfano, unweza kupata vipole vya kuwasha au ulimi wako unaweza kuwa mkubwa.

## Madhara makubwa lakini ya adimu




Madhara makubwa yanajumuisha:

- kuhisi vibaya au kutapika
- kupata shida ya kupumua




- **kupumua kwa shida** – inamaanisha unapiga sauti ambayo si ya kawaida kusikia unapopumua
- kujisikia mapigo haraka ya moyo
- maumivu katika mguu wako
- kuanguka chini au kupoteza ufahamu.

## Madhara adimu ila ya hatari: kuganda kwa damu



Madhara mengine ya hatari ni kuganda kwa damu. Damu inapoganda na kushikilia pamoja, tunaita hiyo kuganda kwa damu.



Hali adimu hii inaweza kusababisha ulemavu mkali wa muda mrefu au kifo. Lakini kuganda huko kwa damu kunaweza kutibwa kwa ufanisi.

Dalili za madhara hayo adimu zinaweza kujumuisha:



- maumivu mabaya sana ya kichwa:
  - yanayoanza angalau siku 4 baada ya chanjo yako
  - hayaponi ikiwa unatumia dawa ya maumivu
  - yanazidi kuwa mabaya unapolala chini.




- Kushindwa kuona vizuri
- kuwa vigumu kuongea
- kifafa



- maumivu katika kifua chako au mguu



- maumivu tumboni yasiyokwisha



- madoa madogo chini ngozi yako ambayo si karibu na mahali ambapo sindano iliingia mkononi wako.

## Ufanye nini ikiwa unajisikia madhara?



Ikiwa unapata mojawapo ya **madhara makubwa** hayo au athari **kali** ya kuzia baada ya kuwa umepata chanjo ya COVID-19, unapaswa kupiga simu ambulensi kwenya 000 moja kwa moja.



Ikiwa unapata madhara yoyote ya **kawaida** ambayo yanakusumbua, unaweza kutumia dawa za kupunguza maumivu.


Dawa rahisi za kupunguza maumivu kama paracetamol au ibuprofen inaweza kuwa nzuri kwako.



Zungumza na daktari wako kabla hujatumia aina zozote zingine za dawa za kupunguza maumivu.



Unaweza pia kutumia begi ya baridi kwa mkono wako mahali ambapo sindano iliingilia.



Zungumze na daktari wako ikiwa wewe:

- una wasiwasi juu ya madhara
- unapata athari ya kuzia
- una madhara yanayoendelea kwa zaidi ya siku 1 hadi 2
- una madhara yanayoanza siku 4 hadi 28 baada ya chanjo yako
- una madhara ambayo sio katika karatasi hii ya ukweli.

Je, unahitaji kupata kipimo cha **COVID-19** baada ya chanjo?



Baadhi ya madhara ya chanjo yanafanana na **dalili** za ugonjwa wa COVID-19. Dalili ni alama zinazoonyesha kwamba labda unaumwa.



Watu wengine wanaweza bado kupata ugonjwa wa COVID-19 baada ya chanjo yao.





Unapaswa kupata kipimo cha COVID-19 ikiwa una dalili zozote za ugonjwa wa COVID-19, kujumuisha:

- homa
- uchovu



- maumivu ya koo
- kikohozi
- upungufu wa pumzi
- kupoteza hisia ya kuonja
- kupoteza hisia ya kunusa.



Pia utaweza kuhitaji kipimo cha COVID-19 ikiwa:

- mtu ambaye umemwona hivi karibuni amepata ugonjwa wa COVID-19
- unakaa katika jimbo au wilaya yenye kesi nyingi za COVID-19.



Ikiwa huna hakika, zungumza na daktari wako.

## Habari zaidi



Unaweza kutembelea tovuti ya Idara ya Afya kwa [www.health.gov.au/covid19-vaccines-languages](http://www.health.gov.au/covid19-vaccines-languages) kupata habari zaidi juu ya chanjo katika lugha yako.



Unaweza kupiga simu kwa Simu ya Msaada wa Virusi vya Korona ya Kitaifa kwenye **1800 020 080**.

Ikiwa unataka habari katika lugha mbali ya Kiingereza, pigia simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani kwenye **131 450**.